

102/3  
KISWAHILI  
FASIHI  
KARATASI YA TATU  
JULAI / AGOSTI 2013  
MUDA: 2  $\frac{1}{2}$

## MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA NANDI YA KATI 2013

CHETI CHA KUHITIMU MASOMO YA KIDATO CHA NNE  
KISWAHILI  
FASIHI  
KARATASI YA TATU  
MUDA: 2  $\frac{1}{2}$

### MAAGIZO

1. Jibu maswali manne pekee.
2. Swali la kwanza ni la lazima.
3. Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani: Riwaya, Tamthilia, Ushairi, .Hadithi Fupi na Fasihi simulizi.
4. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
5. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

## SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI (SWALI LA LAZIMA)

1. (a) Jadili njia zozote **tano** ambazo jamii ya kisasa hutumia ili kudumisha fasihi simulizi. (alama 10)
- (b) Taja na ueleze **vipengele vitano** vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi. (alama 10)

## SEHEMU YA B: RIWAYA

### UTENGANO (SAID A. MOHAMED)

Jibu swali la 2 au 3

2. "Mimi namjua alivyokuwa zamani, lakini nani asiyekuwa na dosari, kwani hata mimi sina asili wala fasili. Basi sote tumeshakula yamini kusahau yaliyopita. Yeye anajuta na mimi nimekubali.
  - (a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)
  - (b) Kwa kurejelea mazingira mbalimbali fafanua jinsi anayerejelewa alivyokuwa zamani kulingana na msemaji. (alama 6)
  - (c) Fafanua sifa zozote **tatu** za anayeambiwa maneno haya. (alama 6)
  - (d) Eleza mbinu zozote **mbili** za lugha zilizotumiwa katika dondo hili. (alama 4)

AU

3. Huku ukitoa mifano mwafaka, jadili maudhui ya kisasi katika riwaya ya Utengano. (alama 20)

## **SEHEMU C: TAMTHILIA**

***MSTAHIKI MEYA (TIMOTHY AREGE)***

### **Jibu swali la 4 au 5**

4. Jadili mbinu zinazotumiwa na uongozi wa cheneo kukandamiza raia wake na kuendelea kutawala. (alama 20)

AU

5. “Uvundo haswa! Hata hao wageni sijui wataonaje hali hii. Aibu kubwa inatungoja kama watakuja.”

- (a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)

- (b) Fafanua sifa nne za msemaji na maneno haya. (alama 4)

- (c) Kwa kutolea mifano taja mbinu moja ya utunzi inayojitokeza katika dondo hili. (alama 2)

- (d) Mbali na uvundo unaorejelewa katika dondo hili, jadili uvundo mwingine unaojitekeza katika baraza la mji wa Cheneo. (alama 10)

## **SEHEMU YA D: HADITHI FUPI**

***DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE (Ken Walibora na Said A. Mohamed)***

6. “Nashangaa vile kwetu tunavyowaabudu watu hao wasiotujali.”

“Kwetu wapi?”

.....”Ahaa! You guys are our brothers.”

- (a) Weka dondo hili katika muktadha wake. (alama 4)

- (b) Taja na ueleze mbinu mbili za lugha zilizotumika katika dondo hili.(alama 4)

- (c) Jadili sifa zozote **tatu** za wazungumzaji katika dondo hili. (alama 12)

### **SEHEMU YA E: USHAIRI**

7. Na ujenge nyumba yako, jingi jasho likuoshe,  
Ufyeke, upime na uweke nguzo,  
Kisha paa uweke na ukandike,  
Siku nyingi bila kuingiliwa na mgeni hutakaa.

Wataanza kutalii mpaka mende usiku,  
Nje na ndani ya nyumba watazunguka,  
Bila woga, bila ruhusa ulichonacho watakula,  
Masalia yatakuwa yako, ijara ya kaziyo.

Na nyingi dawa uweke, nyumba nzima uihame,  
Ukae nje nzima siku usubiri,  
Wazima wamelala ukirudi usiku,  
Vichwa vigumu hawafi mende rahisi.

Kifo cha mende sharti miguu juu  
Kichwa ukikanyage kipasuke usikie,  
Na kisha wengine usiku mchana uwasake.  
Mpaka watakapokwisha. Usiseme nao.

### **Maswali**

- (a) (i) Hili ni shairi la aina gani? (alama 1)  
(ii) Tetea jibu lako. (alama 3)
- (b) Eleza jinsi mshairi alivyoutumia uhuru wake katika utunzi wa shairi hili. (alama 4)
- (c) Taja mbinu mbili za lugha alizotumia mshairi na uzitolee mifano. (alama 4)
- (d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (alama 4)
- (e) Eleza ujumbe wa mshairi. (alama 2)
- (f) Toa mfano mmoja wa mshata. (alama 1)
- (g) Kichwa gani kinaliafiki shairi hili? (alama 1)